



STATE OF MICHIGAN

GRETCHEN WHITMER  
GOVERNOR

OFISI YA GAVANA

GARLIN GILCHRIST II  
LT. GOVERNOR

## AGIZO LA MTENDAJI

No. 2020-4

### TAMKO LA HALI YA DHARURA

Virusi vya corona (COVID-19) ni ugonjwa wa upumuaji ambao unaleta umahututi nakifo virusi vinavyoathiri mfumo wa upumuaji ambavyo vinaweza kukusababisha kuwa mahututi na kufa. Vinasababishwa na aina mpya ya virusi vya corona ambavyo havijawahi kutambulika hapo kabla kwa wanadamu na vinasambazwa kirahisi kutoka mtu mmoja kwenda kwa mwingine.

COVID-19 imetambulika kama sababu ya mlipuko wa ugonjwa unaoathiri mfumo wa upumuaji ambao kwa mara ya kwanza uligunduliwa katika mji wa Wuhan, Mkoa wa Hubei nchini China. Maambukizi ya mtu kwa mtu ya virusi vya ugonjwa huu yamepatikana nchini Marekani na baadhi ya hayo maambukizi yamepatikana kwa watu wasiokuwa na historia ya kusafiri na haijulikani chanzo cha malipuko yalipotokea. Mwezi wa Kwanza, tarehe 31, 2020, Katibu wa Idara ya Afya na Huduma za Binadamu wa Marekani Alex Azar alitoa tangazo la dharura kwa afya ya umma ya COVID-19, ambayo imeathiri mkoa/jimbo na serikali za mitaa, na serikali tawala pia zimetangaza hali ya dharura.

Jimbo la Michigan imechukua hatua za haraka za kujizuia na kujiandaa kwa kuenea kwa ugonjwa huu. Mwezi wa Pili, tarehe 3, 2020, Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ya Michigan (MDHHS) ilikifungua tena kituo cha Utaratibu wa Dharura ya Afya ya jamii, na imekuwa ikifanya kazi kwa bidi na idara za afya za mitaa, mifumo ya afya, na watoa huduma za matibabu sehemu zote za Michigan na inahakikisha uchunguzi sahihi na maandalizi ya COVID-19 yanafanywa. Mnamo mwezi wa Pili 28, 2020, nilianzisha tena Kituo cha upasuaji Oparesheni cha Dharura cha Jimboni ili kuongeza ushirikiano na mkoa, mitaa, mashirika ya serikali, na pia mashirika binafsi, na kusaidia kuzuia kuenea kwa ugonjwa huu. Mnamo Machi 3, 2020, niliunda vikosi vine vya kazi vinavyojumuisha mashirika muhimu ya serikali kushirikiana na wito wa Jimbo na kufanya kazi kwa karibu na jamii husika na wadau wasio wa serikali kupambana na kuenea kwa COVID-19 na kukagua athari inayoweza kuletwa kwenye maisha ya kila siku ya wananchi wa Michigan. Na kwa wakati huo wote, Jimbo limekuwa likishirikiana na shule, biashara, watoa huduma za matibabu, idara za afya za mitaa, na wakazi kuhakikisha wana habari wanazohitaji kwa ajili ya kujiandaa na kesi zinazoweza kutokea.

Mnamo mwezi Machi 10, 2020, MDHHS ilizitambua kesi mbili za kwanza zilizobainika kuwa na maambukizi ya COVID-19 hapa Michigan.

Kifungu cha 1 cha ibara ya 5 ya Katiba ya Michigan ya mwaka 1963 inampa nguvu ya Utendaji Gavana wa Michigan.

Sheria ya Usimamizi wa Dharura ya mwaka 1976 PA 390, kama ilivyorekebisha, MCL 30.403(4), inasema kuwa “Gavana ana uwezo, kwa agizo la utendaji au maelekezo, kutangaza hali ya dharura ikiwa ataona kuwa kuna dharura imetokea au kwamba kuwepo kwa tishio la dharura

Sheria ya Uwezo wa Gavana ya Dharura ya mwaka 1945, 1945 PA 302, kama ilivyorekebisha, MCL 10.31(1), inasema kwamba “wakati wa shida kubwa za migogoro, majanga, ghasia, maafa, au dharura ya umma sawa na zilizotajwa ndani ya jimbo, au hofu inayokubalika ya aina hizo iletayo hatari ya umma... Gavana anaweza kutangaza hali ya dharura na kutaja eneo husika.”

Kupitia Katiba ya Michigan ya mwaka 1963 na sheria ya Michigan, naagiza yafuatayo:

1. Hali ya dharura imetangazwa kwenye Jimbo lote la Michigan.
2. Usimamizi wa Dharura na Usalama wa ndani ya nchi kwenye Kitengo cha Polisi wa Jimbo lazima washirikiane na kuongeza juhudi zote jimboni ambazo zinaweza kuanzishwa kwenye huduma za jimboni ili ziweza kusaidia serikali za mitaa na maafisa na wanaweza kuungana na idara zote za Jimboni kutumia rasilimali zilizopo ziweze kusaidia.
3. Hali ya dharura husimamishwa endapo viashirio vya dharura vitakuwa havipo na mipango sahihi itekelezwe kuleta unafuu baada ya athari ya hali ya dharura, kuambatana na mamlaka za sheria ambazo tamko hili limetolewa na mipaka ya muda iliyowekwa na mamlaka hiyo.

Imetolewa chini ya mknono wangu na kusainiwa na Muhuri Mkuu wa Jimbo la Michigan

  
GRETCHEN WHITMER

Tarehe: Machi 10, 2020

GAVANA

Kutoka kwa Gavana:

  
SECRETARY OF STATE

ON 3/10/2020 AT 11:30pm



IMEJAZWA NA KATIBU WA JIMBO